

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



## OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

### HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI



*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na KMC/ M.13 /6/72**

**20 Septemba, 2021**

### TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Manispaa Kinondoni amepokea kibali cha ajira ya mkataba yenye Kumb Na. FA .170/374/01/ "A"/38 ya tarehe 15/06/2021 kwa kada ya Madereva yenye idadi ya nafasi thelathini na tisa (39) Kutoka kwa Katibu Mkuu menenejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, **Nafasi 36** zimeshajazwa na kubaki **nafasi tatu 3**.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni anakaribisha maombi ya kazi ya Ajira ya Mkataba wa muda kwa kada ya Madereva kutoka Kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi wazi za kazi **3** kama ilivyobainishwa katika Tangazo hili.

#### **1.0 DEREVA DARAJA LA II TGS B - (NAFASI 3)**

##### **1.1 MAJUKUMU YA KAZI**

- i) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari,
- ii) Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi,
- iii) Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari,
- iv) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali,
- v) Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari,
- vi) Kufanya usafi wa gari, na
- vii) Kufanya kazi nyingine kadri anavyoelekeza na Msimamizi wake

## 1.2 SIFA ZA MWOMBAJI


- i. Kuajiriwa kwenye Cheti cha Kidato cha NNE (Form IV) na leseni ya Daraja la E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka bila kusababisha ajali.
- ii. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- iii. Waombaji wenye Cheti cha Majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

## 1.3 MSHAHARA

Kuzingatia Ngazi ya Mishahara ya Serikali TGS B

## 1.4 MASHARITI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45
- ii. Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI
- iii. Picha moja "Passport size" ya hivi karibuni
- iv. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.
- v. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (**Detailed C.V**) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (**referees**) watatu wa kuaminika.
- vi. **Testimonials**", "**Provisional Results**", "**Statement of results**", hati matokeo za kidato cha nne na sita (**FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS**) **HAVITAKUBALIWA.**
- vii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU au NECTA).
- viii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- ix. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 04 Oktoba , 2021.
- x. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili hayatafikiriwa
- xi. Maombi yawasilishwe Kwa njia ya barua posta kwa mkurugenzi wa manispaa S.L.P 31902 Kinondoni.

  
Hanifa Suleiman Hamza

**MKURUGENZI WA MANISPAA**